

UTARATIBU WA KUPATA LESENI YA BIASHARA YA MIFUGO HAI

Fomu ya Maombi ya Leseni za Biashara (TFN 211) kwa biashara ya kununua na kusafirisha Mifugo yanatakiwa kuambathishwa na nyaraka zifuatazo (*Dully filled application Form (TFN 211) for Buying and Transportation of Livestock business license shall be accompanied by the following documents*):-

1. Mtu Binafsi

A: Biashara ya Mifugo katika Mkoa

Mfanyabiashara anayefanya biashara ya kununua na kusafirisha mifugo yaani katika minada ya awali ndani ya mkoa anapaswa kuwa na vielelezo vifuatavyo:-

- Kutambuliwa na kusajiliwa na Bodi ya Nyama kupitia Idara ya Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya/Manispaa husika kwa malipo ya shilingi 62,000/- na kupata Cheti Cha Usajili wa Wadau wa Sekta ya Nyama-Kutoka Bodi ya Nyama Tanzania.
- Kitambulisho cha mwombaji wa leseni.
- Uthibitisho wa Kuwa ana mahali pa Kufanyia biashara (Mfano. Mkataba wa pango wa Ofisi, Leseni ya Makazi au Hati).
- Kuwa na cheti cha Utambulisho wa mlipa kodi TIN kutoka TRA kinatolewa bila malipo
- Kuwa na *Tax clearance* inayokokotolewa TRA.

Mfanyabiashara mwenye viambatisho husika atapewa Leseni ya kufanya biashara ya Mifugo ndani ya Mkoa husika. Leseni inatolewa na Ofisi ya Biashara ya Halmashauri kwa malipo ya kuanzia shilingi 80,000 na kuendelea kulingana na ada iliyopangwa na Halmashauri Husika.

B: Biashara ya Mifugo ndani ya nchi - Tanzania Bara

Mfanyabiashara anayefanya biashara ya kununua na kusafirisha mifugo ndani ya nchi yaani katika minada ya awali, upili na mipakani anapaswa kuwa na vielelezo vifuatavyo:

- Kutambuliwa na kusajiliwa na Bodi ya Nyama kupitia Idara ya Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya/Manispaa husika kwa malipo ya shilingi 62,000/- na kupata Cheti Cha Usajili wa Wadau wa Sekta ya Nyama-Kutoka Bodi ya Nyama Tanzania.
- Kitambulisho cha mwombaji wa leseni.
- Uthibitisho wa Kuwa ana mahali pa Kufanyia biashara (Mfano. Mkataba wa pango wa Ofisi, Leseni ya Makazi au Hati).
- Kuwa na cheti cha Utambulisho wa mlipa kodi TIN kutoka TRA ambacho kinatolewa bila malipo
- Kuwa na *Tax clearance* inayokokotolewa TRA.

Mfanyabiashara mwenye viambatisho husika atapewa Leseni ya kufanya biashara ya Mifugo ndani ya nchi - **Tanzania Bara** kutoka BRELA kwa malipo ya shilingi 200,000.

Endapo atahitaji huduma nyingine BRELA kama vile;-

- Kusajili jina la biashara atalipa kiasi cha shilingi 22,000
- Kusajili Kampuni malipo yatategemea na kiwango cha mtaji wa biashara ambayo yanaanzia shilingi 160,000 hadi 720,000.

Maombi yote yawasilishwe kwenye Ofisi ya Leseni za Biashara zilizopo Jengo la Ushirika Ghorofa Na. 5 Mtaa wa Lumumba, Mnazi Mmoja Dar es Salaam.

C: Biashara ya mifugo nje ya nchi

Mfanyabiashara anayefanya biashara ya mifugo nje ya nchi yaani kutoka minada ya mipakani kwenda nje ya nchi anapaswa kuwa na vielelezo vifuatavyo:-

- Kutambuliwa na kusajiliwa na Bodi ya Nyama kupitia Idara ya Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya/Manispaa husika kwa malipo ya shilingi 152,000/- na kupata Cheti Cha Usajili wa Wadau wa Sekta ya Nyama- Kutoka Bodi ya Nyama Tanzania.
- Kitambulisho cha mwombaji wa leseni.
- Uthibitisho wa Kuwa ana mahali pa Kufanyia biashara (Mfano. Mkataba wa pango wa Ofisi, Leseni ya Makazi au Hati).
- Kuwa na cheti cha Utambulisho wa mlipa kodi TIN kutoka TRA kinachotolewa bila malipo
- Kuwa na *Tax clearance* inayokokotolewa TRA

Mfanyabiashara mwenye viambatisho husika atapewa Leseni ya kufanya biashara ya Mifugo nje ya nchi kutoka BRELA kwa malipo ya shilingi 300,000.

Endapo atahitaji huduma nyingine BRELA kama vile;-

- Kusajili jina la biashara atalipa kiasi cha shilingi 22,000
- Kusajili Kampuni malipo yatategemea na kiwango cha mtaji wa biashara ambayo yanaanzia shilingi 160,000 hadi 720,000

Maombi yote yawasilishwe kwenye Ofisi ya Leseni za Biashara zilizopo Jengo la Ushirika Ghorofa Na. 5 Mtaa wa Lumumba, Mnazi Mmoja Dar es Salaam.

2. Kampuni na Majina ya Biashara

Iwapo ni Kampuni ndiyo inayoomba leseni ya ngazi yoyote inapasawa kuwa na nyaraka/vielelezo vifuatavyo:-

- Hati ya kuandikishwa kama Kampuni (Certificate of Incorporation); Jina la Biashara (Certificate of Registration and Extract),
- Memorandum and Articles of Association/Mkataba wa Makubaliano kati ya Wabia (Partnership deed);
- Cheti Cha Usajili wa Wadau wa Sekta ya Nyama-Kutoka Bodi ya Nyama Tanzania,
- Hati ya mlipa kodi (Tin Number);
- Tax clearance certificate) kutoka TRA;
- Mkataba wa pango yenye mihuri ya mwanasheria na kodi ya TRA iwe imelipwa (Lease Agreement with advocate stamp and TRA stamp duty paid); na,
- Uthibitisho wa uraia kwa wenye hisa (Proof of shareholder's citizenship)